

P.O.BOX 11836
Office phone: +255685 781 028
+255678 0211 811
Dar-es-Salaam
Tanzania
Emails: info.tannahq@gmail.com
info@tanna.or.tz
Website: www.tanna.or.tz



Tanzania National Nurses
Association (TANNA)
Tanna House
Mbezi Beach, Tangi Bovu
Dar-es-Salaam
Tanzania

Date: 16th June 2024

TAARIFA KWA UMMA

Chama cha Wauguzi Tanzania (**TANNA**) *Tanzania National Nurses Association* ni chama cha Wauguzi nchini kilichoanzishwa kisheria chini ya sheria ya uanzishwaji vyama vya kijamii na kitaaluma societies ordinance act, 1954 (rule 5). Moja ya Lengo la Chama ni kuimarisha ubora wa huduma za kiuguzi kwa kuhamasisha sera bora zinazolenga kuboresha huduma za afya, kutetea na kuhamasisha wajibu na haki ya Muuguzi katika utoaji wa huduma bora za afya pamoja na kuhakikisha wanataaluma wanatoa huduma bora inayotarajiwa na wateja wetu kwa kuzingatia weledi na miongozo iliyowekwa..

Chama cha Wauguzi Tanzania tunakiri kuona video inayoendelea kusambaa katika mitandao ya Kijamii juu ya tuhuma za mama aliyejifungulia katika Zahanati ya Basanza iliyopo Kijiji cha Basanza, kata ya Basanza Wilayani Uvinza bila ya Usaidizi wa mtaalamu wa Afya.

Katika ufatiliaji uliofanywa na Viongozi wa Chama cha Wauguzi Tanzania wa ngazi mbalimbali, umebaini ya kuwa mama huyo alifika Zahanati ya Basanza Tarehe 09/06/2024 akitokea kwenye maabara binafsi iliyopo katika kijiji cha Basanza kwa ajili ya kupata huduma za vipimo kutokana na maumivu ya tumbo aliyokua nayo pasipo kufahamu ya kuwa maumivu hayo yanababishwa na uchungu, lakini kabla ya kupatiwa huduma maumivu yalizidi ndipo alipoamua kwenda Zahanati ya Basanza na kupitiliza katika chumba cha kujifungulia wazazi (labour Ward) na kwakua alishakua na uchungu wa muda mrefu alifika tu na kujifungua moja kwa moja.

Muuguzi aliyejukwepo zamu alishinda toka asubuhi kituoni na kwakua hapakuwa na mgonjwa ye yote yule majira ya saa 10 jioni alitoka kwenda nyumbani kwake ambapo ni karibu na kituo (takribani mita 5 tu) kwa lengo la kujipatia huduma ya chakula cha mchana, ndipo huku nyuma mzazi huyo akaingia na mmewe ambaye alilazimika kutoka kutafuta msaada wa Muuguzi huku mwananchi mwингine wa kiume akiingia katika chumba hicho na kumrekodi mama huyo pasipo mtu ye yote kutambua. Hata hivyo Muuguzi huyo alipopata taarifa akasitisha zoezi la kula na kufika kituoni na kukuta mama huyo ameshajifungua mtoto wa kiume akiwa mzima wa afya na mwenye uzito wa

kilo 2.6. Mzazi huyo alipatiwa huduma zote muhimu za Kiuuguzi na Ukunga na kupunzishwa hadi siku ya tarehe 10 June, 2024 mchana aliporuhusiwa kwenda nyumbani akiwa salama yeye pamoja na mtoto wake. Aidha na tayari mama huyo ameshshudhuria hudhurio la kwanza tarehe 14.06.2024 kwa ajili ya huduma za chanjo na ufatiliaji wa Afya ya mama baada ya kujifungua kama alivyoelekezwa na Muuguzi huyo.

Chama cha Wauguzi Tanzania (TANNA), Tunasikitishwa na Tunakemea vikali sana vitendo vinavyofanywa na baadhi ya Wananchi wasio na lengo jema kwa kuingia mpaka vyumba vyaa faragha vyaa huduma na kurekodi wateja hali inayovunja haki ya Utu na usiri wa Afya ya mteja, kuchonganisha Watumishi, Serikali na Wananchi lakini la zaidi kusababisha taharuki katika jamii. Ikumbukwe mnamo tarehe 28 May, 2024 ilisambaa video nyingine iliyochochukuliwa kwa siri na Mwananchi inayomwonesha mama aliyefahamika kwa jina la Rehema aliyekua amepumzika nje katika Kituo cha Afya Gungu kilichopo katika Halmashauri ya Manisapaa Kigoma Ujiji huku habari iliyotolewa ikisema "**MGONJWA KUFUKUZWA NA WAUGUZI KIGOMA**" wakati uhalisia mteja huyo alikuwa akisubiri usafiri wa kurudi nyumbani baada ya kupata huduma.

Chama cha Wauguzi Tanzania, tunaiomba Serikali kuwachukulia hatua wananchi wanaotoa taarifa chonganishi kama hizi na kuzua taharuki, lakini pia kuwaelekeza Wananchi namna bora ya uwasilishaji malalamiko ya huduma kuititia njia sahihi zilizowekwa na Serikali, pia tunaendelea kuwasihhi wanachama wetu kuendelea kutoa huduma bora za Uuguzi na Ukunga kwa kuzingatia misingi ya taaluma yetu inavyotuelekeza.

Imetolewa na,

CHAMA CHA WAUGUZI TANZANIA (TANNA)